# HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME
# PROF. WILLY LAZARO KOMBA
# KATIKA UZINDUZI WA TOVUTI MPYA YA TUME
# IJUMAA MEI 27, 2022 JIJINI DODOMA
# KATIKA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE CONVENTION - DODOMA.

Waheshimiwa Makamishna wa Tume;

Ndugu Katibu wa Tume;

Wajumbe wa Menejimenti ya Tume;

Wajumbe wa Kamati ya TEHAMA;

Mtaalamu mwakilishi kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA);

Ndugu Sekretarieti;

Wanahabari;

Mabibi na Mabwana na

Watumishi wengine wote wa Tume mliojumuika pamoja nasi hapa leo katika shughuli hii fupi ya uzinduzi wa tovuti mpya ya Tume;

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

**Ndugu washiriki wa hafla hii;**

Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai na afya njema kuweza kukutana hapa leo na muda huu kwa shughuli hii muhimu kwa utekelezaji wa majukumu yetu ya Tume, utoaji huduma kwa Walimu tunaowahudumia, Wadau mbalimbali wa Tume, Wananchi na Taifa kwa ujumla.

**Ndugu washiriki;**

Kama sote tulivyosikia maelezo ya awali ya mwenendo wa tovuti ya Tume tangu mwaka 2017 mpaka sasa katika utekelezaji wa majukumu ya Tume tuliyokasimiwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, tumesikia changamoto kadhaa ambazo zimekua zikikwamisha upakiaji na uhuishaji wa taarifa na mambo mbalimbali ambayo Tume ingependa yawafikie walengwa na jamii kwa ujumla kwa wakati tarajiwa ili kufikia malengo ya utekelezaji.

Tangu Tume kuwa na tovuti mwaka 2017 mpaka sasa 2022 ni miaka saba (7) ambapo tangu tuwe na tovuti kwa msaada wa wadau wa maendeleo, watu **182,650** tu walipata kuitembelea tovuti yetu. Idadi hii ni ndogo kulingana na matarajio ya TUME. Kwa kiasi kikubwa changamoto zilizokuwepo zilikuwa zinaathiri ufanisi wa tovuti kutokana na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia duniani katika eneo la Habari, Elimu, Mawasiliano na Uhamasishaji.

**Ndugu washiriki;**

Baada ya kupata tovuti hii mpya ambayo itaanza kutumika mara baada ya uzinduzi huu hapa; naelekeza na kusisitiza Maafisa husika wa Tume katika uendeshaji wa tovuti hii pamoja na zana nyingine za uhabarishaji, uelimishaji na uhamasishaji ikiwemo mitandao ya jamii rasmi ya Tume, kuzingatia viwango, maelekezo na miongozo yote ya Serikali katika njia na zana zote za Mawasiliano na jamii.

Imeelezwa kuwa tovuti hii inaendana na hali halisi ya sasa ya mabadiliko ya kiteknolojia. Maafisa TEHAMA, Habari na Mawasiliano ya Serikali wa Tume wamewezeshwa kuwa na umiliki wa moja kwa moja wa tovuti hali

inayosababisha uhuishaji wa taarifa na kufanya maboresho mbalimbali kwa wakati. Ni matumaini yangu kuanzia sasa taarifa zote hai zenye tija kwa Walimu, Wateja, Wadau na Jamii kwa ujumla wake zitapatikana kwa wakati zikiwa hai na zenye tija kwa walengwa ikiwa ni pamoja na kuwezesha wateja kupata huduma muhimu za Tume kupitia tovuti hii bila kulazimika kutembelea Ofisi za Tume Makao Makuu au katika Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya zote 139.

**Ndugu washiriki;**

Imeelezwa hapa kuwa; Tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa chanzo sahihi na bora kwa Walimu, Wateja na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Elimu kupata taarifa mbalimbali za Tume. Ni wazi taarifa na maudhui yatakayowekwa kwenye tovuti yatatumika kwa usahihi katika kazi mbalimbali ikiwemo kujifunza, kufanya tafiti, kupata huduma na rejea ya nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Utumishi wa Walimu. Nawasihi wadau wote hususan walimu kuitumia tovuti hii kupata huduma, taarifa, maudhui, takwimu na nyaraka mbalimbali kwa rejea na matumizi sahihi.

**Ndugu washiriki;**

Nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha zoezi hili la kutengeneza tovuti hii ambalo lilianza baada ya maelekezo ya Tume kwa Menejimenti kupitia Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali.

Nawashukuru sana Wadau wa Maendeleo ambao ndiyo msaada na chanzo cha awali cha kuifanikisha Tume kuwa na tovuti ambayo ndicho chombo na zana kuu ya uhabarishaji wa shughuli na majukumu ya Tume.

**Ndugu washiriki;**

Kipekee niwashukuru sana Makamishna kwa ushirikiano wao na Wajumbe wa Menejimenti kwa utekelezaji wa jambo hili kwa wakati. Hali kadhalika Kamati ya TEHAMA ya Tume kwa maoni na ushauri wao, Idara na Vitengo vyote kwa kuwezesha mchakato wa kumpata mzabuni wa kutufanyia kazi hii ikiwa ni pamoja na kuandaa maudhui na taarifa mbalimbali ambazo zitatumika kwenye tovuti hii.

**Ndugu washiriki;**

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, niwapongeze Kitengo cha TEHAMA na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kwa kuratibu zoezi la matengenezo ya tovuti hii kwa pamoja na Watalaam wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ambao pia ndio wazabuni watekelezaji kwa ushauri na kazi kubwa ya kutengeneza tovuti hii pamoja na kuwapa mafunzo Maafisa Watalaam wa Tume ya namna ya kusimamia na kuhuisha taarifa.

**Ndugu washiriki;**

Kwa kuwa matumizi rasmi ya tovuti hii mpya yataanza mara baada ya uzinduzi kwa kuitoa hewani ile ya zamani na kuipandisha hewani hii mpya; basi nichukue fursa hii sasa kuizindua rasmi tovuti hii. ***(Kubofya kitufe cha uzinduzi rasmi…..).***